Swahili

## Je, ulijua?

# Kaswende ni maambukizo makubwa ambayo yanaweza kudhuru kila mtu.



## Pata kipimo, utibiwe na upone!

Bila matibabu, kaswende inaweza kuathiri sana afya yako.

### Huenda usiwe na dalili zozote

Mtu yeyote anaweza kupata kaswende – ambayo ni aina ya maambukizo ya zinaa (STI).

Huenda usijue kuwa unayo. Pata kipimo mara kwa mara ili kujiweka salama wewe na wengine.

### Pimwa, utibiwe na upone!

Matibabu ya kaswende ni rahisi.

Omba daktari yako au tembelea kituo cha kimatibabu ili kupata kipimo kamili cha STI ambacho kinajumuisha kaswende, hata ikiwa huna dalili.

### Huduma ya ujauzito

Ikiwa wewe ni mja mzito au unapanga kuzaa mtoto, kupimwa mapema ni muhimu sana ili kuhakikisha huambukizi kaswende kwa mtoto wako.

### Kaa salama

Njia nzuri sana kuzuia kaswende ni kufanya ngono salama – kila wakati tumia kondomu na tumia vilainishi vyenye maji au vya silikoni.

Wapenzi pia wanapaswa kupimwa mara kwa mara ili kuzuia kaswende kurudi kwako au kuwaambukiza wengine.

### Kuzungumza na muuguzi aliyefunzwa

Piga simu kwa Simu ya Maelezo ya Afya ya Kingono (SHIL) kwa **1800 451 624** Jumatatu hadi Ijumaa (Monday-Friday) Saa 3.00 asubuhi hadi Saa11.30 jioni (9:00am to 5:30pm).

Piga simu kwa **131 450** kuzungumza katika lugha yako. Inapatikana siku 7, masaa 24.

Tembelea tovuti kwa **www.shil.nsw.gov.au**

Changanua msimbo wa QR ili kujua zaidi kuhusu kaswende na afya ya wanawake.

MULTICULTURAL HIV & HEPATITIS SERVICE

**Wilaya ya Afya ya Mahali ya Sydney ya Kusini Magharibi**
Huduma ya Kukuza Afya

NSW GOVERNMENT